

TANGAZO LA ZABUNI

ZABUNI YA UWAKALA WA USAFI WA MAZINGIRA HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA

1. Halmashauri ya Mji wa Bunda inakusudia kupata wazabuni wenye uwezo wa kukusanya ada za taka, kufanya Usafi wa Mazingira, Kuzoa taka na kuzisafirisha kwenda dampo la Migungani kutoka katika maeneo ya Makazi, Biashara, Masoko, Maeneo ya wazi na Taasisi mbalimbali katika Halmashauri ya Mji wa Bunda kwa kipindi cha kuanzia tarehe 01 Machi 2024 hadi tarehe 1 Machi 2025,
2. Halmashauri ya Mji wa Bunda inapenda kuwaalika **wakandarasi, Watu Binafsi, Makampuni, Mashirika, Vikundi au Taasisi za umma zilizosajiliwa kisheria**, wenye nia na uwezo wa kufanya kazi hizo kutuma maombi yao kwa zabuni kama ifuatavyo :-

A: UWAKALA WA USAFISHAJI WA MAZINGIRA utajumuisha mafungu yafuatayo; +

- **Fungu I:** Kata ya Bunda Mjini.
- **Fungu II:** Kata ya Balili .
- **Fungu III:** Kata ya Manyamanyama .
- **Fungu IV:** Kata ya Nyamakokoto.
- **Fungu V:** Kata ya Nyasura.
- **Fungu VI:** Kata ya Kabarimu.

KUMBUKA

Mwombaji anaruhusiwa kuomba fungu moja au zaidi na kilafungu atakalo omba ainishe asilimia ya fedha atakazo lipwa kutokana na makusanyo ya ada za taka.


MASHARTI YA JUMLA KWA ZABUNI ZOTE

1. Nakala ya leseni hai (isipokuwa CBO's hazihusiki na sharti hili).
2. Waombaji wote waambatanishe nakala za usajili wa Makampuni yao au Vikundi vya Kijamii (CBOs) au Taasisi.
3. Vikundi vya Kijamii (CBOs) viambatanishe orodha ya viongozi wa kikundi na barua za utambulisho kutoka katika Kata husika.
4. Waombaji wote waambatanishe nakala za VAT au TIN.

5. Mwombaji ni lazima aambatanishe wasifu wa kampuni (Company Profile) au Kikundi CBO's Profile au taasisi.
6. Waombaji wawe na vithibitisho vya kuwa na vifaa vya kazi kama magari/ Trekta kwa kusafirishia taka kwenda dampo, Vifaa vya kutosha vya kusafishia, wafanyakazi/vibarua wa kutosha kutokana na ukubwa wa eneo, pamoja na ofisi ya kudumu. Au aeleze kwa kuambatanisha uthibitizo kuwa amekubaliwa kukodi au atatumia magari ya Halmashauri ya Mji wa Bunda
7. Ili kuhakikisha afya na usalama kwa wafanyakazi watatakiwa kupima afya zao mara mbili kwa mwaka na pia wawe na vifaa kinga "personal protective equipments" (kama vile;-Vizua harufu mbaya).
8. Muombaji/waombaji anatakiwa kuwasilisha picha za Mkurugenzi /Wakurugenzi/Meneja /Mwenyekiti/Katibu wa kampuni yao katika maombi yao.
9. Mwombaji yeyote atakayeshindwa kutimiza au kutokamilisha maelekezo na masharti hayo ya zabuni atakuwa amejiondoa mwenyewe katika ushindani.
10. Halmashauri ya Mji wa Bunda hailazimiki kukubali/ kutokubali kutoa [Award Tender] zabuni kwa mwombaji kutokana na kigezo cha malipo makubwa ya kazi ama huduma iliyoombewa zabuni.
11. Kabrasha la zabuni litatolewa kuanzia tarehe 23/01/2024 siku za kazi na saa za kazi hadi tarehe 24/01/2024 saa nne kamili asubuhi
12. Zabuni zote zifungwe vizuri na juu ya bahasha iandikwe maandishi yanayotaja zabuni, na namba ya zabuni na zipelekwe katika ofisi ya PMU Halmashauri ya Mji wa Bunda. Juu ya bahasha iandikwe zabuni anayo omba. Maombi yote yatumwe kwa: **KATIBU WA BODI YA ZABUNI, HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA. S.L.P 219, BUNDA.**

13. Tarehe ya mwisho wa kupokea maombi ni siku ya **jumatatu ya tarehe 29 mwezi wa kwanza mwaka 2024 Saa 4.30 Asubuhi** na ndiyo siku ya ufunguzi wa zabuni hizi. Waombaji au wawakilishi wao watakaopenda kuhudhuria ufunguzi wanaruhusiwa kuhudhuria.

14. Maombi yatakayofika baada ya muda uliowekwa kuisha hayatapokelewa na hayatafunguliwa.



Emmanuel J. Mkongo,
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
BUNDA